



TRONDHEIM KOMMUNE

Malezi na Elimu

Huduma za Mtoto na Familia





Huduma za Mtoto na Familia (BFT) kwa manispaa ya Trondheim

Huduma za Watoto na Familia imepangwa chini ya Sekta ya manispaa ya Malezi na Elimu, pamoja na shule za mapema na shule. BFT ni kifupisho cha Huduma za Mtoto na Familia.

Huduma na hatua zote hutolewa kulingana na sheria ya Norway ili kuhakikisha kwamba watoto na vijana wanapewa fursa bora za ukuaji wa kiafya.

Wazazi wana jukumu la msingi la kulea watoto wao. Watoto wote wana haki ya kupata elimu ambayo inabadilishwa ili kukita mahitaji yao na uwezo wao. Huduma za Watoto na Familia inafanya kazi pamoja na shule za mapema na shule ili kusaidia wazazi wahakikishe malezi mazuri kwa watoto wao.





Huduma za Watoto na Familia hutoa huduma kadhaa muhimu.

Kituo cha Afya ya Umma / Huduma za Afya Shuleni

Vituo vya afya ya umma vinatoa huduma kwa watoto hadi umri wa miaka sita, na huduma za afya shuleni hutoa huduma kwa watoto na vijana wa kati ya miaka 6 na 20.

Norway ina mpango wa chanjo ya kitaifa, na watoto wote wanachanjwa katika kituo chao cha afya ya umma. Vituo vya afya ya umma hufuatilia ukuaji wa watoto na hutoa msaada na mwongozo kwa wazazi.

Vituo vyote vya afya ya umma na shule vina muuguzi wa afya ya umma, pamoja na daktari na wataalamu wengine wa afya wanaotembea.

Watoto na vijana wanaopambana na shida za kulala, shida za kula, hofu, wasiwasi au shida zingine wanaweza kupata msaada na usaidizi katika kituo cha afya ya umma au kutoka kwa huduma za afya shuleni.



Huduma za Saikolojia ya Kielimu (PPT)

Watoto na vijana watahakikishiwa ukuaji bora zaidi. Watoto wengine wanahitaji msaada kidogo wa ziada. Wakati shule ya mapema au shule ina wasiwasi kuhusu ukuaji wa mtoto, mtoto anaweza kupelekwa kwa Huduma za Elimu ya Kisaikolojia (PPT). Hii inafanywa tu kwa idhini ya wazazi.


PPT husaidia katika kuwezesha huduma bora zaidi za kielimu kulingana na mahitaji na uwezo wa mtoto.

Huduma za Ustawi wa Mtoto

Huduma za Ustawi wa Mtoto itahakikisha kwamba watoto na vijana wanaoishi chini ya hali ambazo zinaweza kuwa na madhara kwa afya zao na ukuaji wanapokea utunzaji unaofaa, malezi na usaidizi. Hii inajumuisha kukita hitaji la mtoto la chakula, mavazi, utunzaji wa kila siku na upendo, pamoja na kutoa mipaka thabiti.

Huduma za Ustawi wa Mtoto hutegemea ushirikiano mzuri na ulio wazi na wazazi. Ni muhimu kutathmini matakwa bora ya mtoto. Huduma za Ustawi wa Mtoto hutafuta kufanya kazi pamoja na wazazi kila wakati





ili kupata suluhisho nzuri kwa mtoto na familia.

Familia zinaweza kuwasiliana na Huduma za Ustawi wa Mtoto moja kwa moja kwa ushauri na mwongozo katika kulea watoto wao.

Wafanyakazi wa shule ya mapema na wa shule, wanafamilia au wengine wanaweza kuwasiliana na Huduma za Ustawi wa Mtoto ikiwa wanajali mtoto. Huduma za ustawi wa watoto inapopokea ripoti ya wasiwasi juu ya hali ya utunzaji wa mtoto, mazungumzo yataanzishwa na mtoto, wazazi, wauguzi wa afya ya umma na wafanyakazi shuleni au katika shule ya mapema.

Pamoja na wazazi na mtoto, Huduma za Ustawi wa Mtoto watatathmini kile kinafaa kufanyika ili kuleta msaada. Katika hali zingine, familia haitahitaji msaada wowote kutoka kwa Huduma za Ustawi wa Mtoto, na katika hali hiyo hakuna usaidizi unaohitajika.

Katika hali zingine, inaweza kuwa muhimu kwa mtoto na wazazi wake kuishi mbali na mwingine kwa muda mfupi au mrefu. Huduma za Ustawi wa Mtoto inaweza kumwondoa mtoto kutoka nyumbani ikiwa, kwa mfano, mtoto yuko hatarini ya kukumbwa na dhuluma au unyanyasaji wa kijinsia, au mfiduo wa dawa za kulevyia katika familia. Lengo la Huduma za Ustawi wa Mtoto ni kuhakikisha afya na usalama wa mtoto kila wakati.

Huduma za Familia

Huduma za Familia zinaweza kutoa ushauri, mwongozo na usaidizi kwa mtu mmoja au kama kikundi cha watoto, vijana na wazazi wao au familia. Wataalam kutoka Huduma za Familia hufanya kazi pamoja na wazazi na hubadilisha huduma zao ili zifikie kila familia ya mtu binafsi. Huduma ni za hiari na familia zinaweza kuwasiliana na ofisi yenye, au kupitia kituo cha afya ya umma, shule ya mapema, shule au daktari wa jumla.

Huduma moja inayotolewa kwa wazazi ni kushiriki katika kikundi cha ICDP. ICDP humaanisha International Child Development Programme (Programu ya Kimataifa kuhusu Ukuaji wa Mtoto). Wazazi huhudhuria mikutano ya kikundi na wazazi wengine ili kubadilishana uzoefu kutoka kwa miingiliano yao na watoto wao. Kusudi ni kufahamu zaidi ni nini bora kwa watoto, na kwa kina mama na baba kujisikia salama zaidi katika majukumu yao ya uzazi. Vipindi vyta kikundi vinategemea uzoefu wa kila siku wa wahusika, na katika hali nyingi, vipindi hufanyika katika lugha ya asili ya wahusika.



Huduma za Makazi / Afya na Utunzaji

Manispaa ya Trondheim imejitolea kuhakikisha huduma zinazofaa na rahisi za ubora mzuri kwa watoto na vijana wenyewe ulemavu na familia zao. Ulemavu unaweza kujumuisha ulemavu wa kuona, kusikia na wa kutembea, shida za kitabia au maswala ya afya ya kiakili. Vijana walio na changamoto hizi wanaweza kuwa na hitaji kubwa la msaada kuliko wenzao.

Wazazi wanaweza kuomba huduma fulani za manispaa, kama anwani ya msaada wa kibinafsi (støttekontakt), usaidizi wa shughuli za burudani, utunzaji wa muda mfupi, malipo ya mtunzaji au ziara za muuguzi wa nyumbani. Huduma za Watoto na Familia itafanya kazi pamoja na wazazi ili kujua mahitaji ya watoto na familia zao, kama vile haki yao ya kupata huduma chini ya sheria za Norway.



Manispaa ya Trondheim
Malezi na Elimu
Postboks 2300 Torgarden
7004 Trondheim

Shukrani kwa
Sedrik, Ylva, Ines, Kjerstin na Andreas; Alia, Ali, Oday, Abir, Aadi, Latifa na Hussin
Picha: Geir Hageskal na Carl-Erik Eriksson
www.trondheim.kommune.no/bft

2019

Kitengo cha Mawasiliano

